

# Sina imani

Nashika yangu kalamu, kumwaga yangu moyoni,

Tulisubiri hukumu, haki lidhani jamani,  
Kumbe yao bure sumu, mashiko hasha kortini,  
Sina imani kortini, sifa tu mlitafuta.

Wale mabwana ukweli, walitafuta kukiki,  
Chaguzi ule halali, wakashau na haki,  
Uchumi na hawajali, litaka sifa miliki,  
Sina imani kortini, sifa tu mlitafuta.

Mwanzoni niliamini, ukweli utadhihiri,  
Tuombeni kwa Manani, atulinde bila shari,  
Tuishini kwa amani, tupendane kwa fahari,  
Sina imani kortini, sifa tu mlitafuta.

Tujengeni nchi yetu, pamoja tuimarike,  
Kabila lisiwe kitu, upendo na uhusike,  
Nyoyoni pasiwe kutu, kununiana sifike,  
Sina imani kortini, sifa tu mlitafuta.

JOSPHAT CHERUIYOT  
Chuo Kikuu SEKU, Kitui